

# DHABIHU

## NDIO JINA LA MCHEZO

Pastor James Kalekwa

# DHABIHU NDIYO JINA LA MCHEZO!

James Kalekwa

## Orodha ya Yaliyomo:

Salamu za Mama Mchungaji JK. ......... 4

Dhana ya Dhabihu ............................ 10

Aina za Dhabihu mtendakazi anatakiwa kutoa ............................................ 12

Dhabihu ya utalaam, ujuzi, maarifa na uzoefu ........................................... 25

Dhabihu ya mali................................ 28

Dhabihu ya nguvu ............................ 33

Dhabihu ya uhai (maisha)................ 35

Dhabihu ya mambo yanayokupendeza na kukupa raha................................ 41

Dhabihu ya ufuasi............................. 44

Kuhusu Mwandishi:.......................... 47

Kuhusu New Vine Church:................ 48

Mawasiliano na Mwandishi:............. 49

# Salamu za Mama Mchungaji JK.

Juni 20, Mungu alitupa zawadi ya maisha ya mtumishi wake Pastor JK, mtu wa juhudi nyingi katika Kristo na maarifa ya kimungu. Kwa muda ambao nimekuwa naye kwenye maisha, nimemtambua kama mtu anayempenda Mungu kiasi cha mimi kukosa neno la kuelezea. Huyu ni mtu aliuzwa kwa Mungu na utumishi!

Amewekeza muda mwingi kuandika mfululizo wa vitabu hivi vya kielektroniki ili avitoe bila malipo kama sehemu yake ya ujenzi wa mwili wa Kristo… kwa niaba yake, ninaomba ukipokee kwa kuthamini dhabihu! Ninakuombea ya kwamba maisha yako

yanageuzwa kwa kitabu hiki kimoja tu kwa jina la Yesu Kristo.

Pili, ninaomba uwasambazie kitabu hiki watu wengi zaidi ili maono ya kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari yatimilizwe.

Na hatimaye, kwa kuthamini zawadi ya mtu huyu wa Mungu, muombee, mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumsherehekea ukimweleza namna gani umesadika na utumishi wake – itafaa sana.

Heri ya siku ya kuzaliwa mume wangu mpenzi. Heri ya kuzaliwa Pastor JK – zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu!

Frida James Kalekwa (Mama mchungaji JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2025

Mara zote Mungu hufungamanisha matokeo makubwa kwenye kazi yake na kifaa kinaitwa kujidhabihu, hivyo matokeo makubwa ni mchakato ambao umehusisha dhabihu kubwa pia.

*Isaya 61:6SUV "Bali ninyi mtaitwa makuhani wa Bwana; watu watawaiteni wahudumu wa Mungu wetu; mtakula utajiri wamataifa, na kujisifia utukufu wao."*

*Ufunuo 5:12-13SUV "wakisema kwa sauti kuu, Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka. Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na*

*vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele''*

Usiingie kwenye mtego wa kutamani kustahili bila ya kulipia gharama tambua kwamba mwanakondoo amestahili kwa sababu amechinjwa hivyo kama hakuna kuchinjwa hakuna kustahili kwa namna yoyote ile.

Kama mtendakazi unapaswa kutambua kuwa hakuna kitu cha bure kwenye ufalme wa Mungu na hivyo ni lazima ulipe gharama ili upate thawabu stahiki.

Kila kuchinjwa kunaambatana na;

i. Uweza
ii. Utajiri
iii. Heshima
iv. Nguvu
v. Utukufu

Muunganiko kati ya Neno la Mungu na utumishi wa kujidhabiju

Nyakati zote utumishi wa kujidhabihu ni matokeo ya hali ya moyo; namna ambavyo moyo umefinyangwa na Neno kuhusu kujitoa kuelekea utumishi matokeo yake huwa ni dhabibu yaani kufanya zaidi ya ilivyotarajiwa.

Mungu anamtarajia mtendakazi awe kifaa akinachofanya zaidi ya kawaida (amplifier and booster) kwenye kila jambo analolileta duniani. Nimewahi kusema kwenye darasa la watendakazi mahali ninapochunga kuwa Mungu ameumba nyanya, vigunguu, hoho, kabeji lakini utaona kuna mtu anakula kachumbari (salad) ya nyanya na vitunguu na mwingine anatengeneza salad. Tofauti zao sio malighafi bali ni ufahamu wao kuhusu malighafi hizo zilizo mbele yao. Nataka nikwambie mtendakazi tumia malighafi ambayo ni Neno la Mungu kuzalisha matokeo makubwa mahali ulipo vitu vyote unavyovihitaji kutokeza matokeo

makubwa unavyo tumia Neno la Mungu livifumue hivyo vitu ndani yako.

## Dhana ya Dhabihu

Dhabibu ni nini?

Dhabihu ni neno ambalo lina maana ya kutenda zaidi ya kawaida, zaidi ya mazoea, zaidi ya matarajio pia kutenda zaidi ya wengine wanavyotenda.

Dhabihu inapinga na huwa inaua ukawaida, mara zote ukawaida na dhabihu havikai pamoja ni maadui wakubwa.

*Marko 14:35SUV"Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akiomba ya kuwa, ikiwezekana, saa hiyo imwepuke"*

Katika muktadha huu dhabihu inadai kanuni ya kuendeleza mbele kidogo yaani zaidi ya wengine.

Dhabihu ni kutenda bila ya kujihurumia wakati inaumiza.

Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifulifuli, akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe.

*Mathayo 26:39SUV "Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifulifuli, akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe*"

## Aina za Dhabihu mtendakazi anatakiwa kutoa

Dhabihu ambazo mtendakazi anapaswa kuzihusianisha na neno la Mungu ili kazi ya Mungu iende mbele na kuwa na tija.

***Dhabihu ya maombi***

Mtendakazi ni kifaa ambacho Mungu huwa anakitumia kutokeza matokeo kwa njia ya maombi. Mtendakazi anawajibu wa kuomba zaidi ya kawaida yaani kupita washirika; mtendakazi anapaswa kutenga muda wa kuomba kwa ajili ya maisha ya watu wengine na zaidi ana wajibu wa

kuliombea kanisa na pia kuwaombea viongozi walio juu yake. Mtendakazi anapaswa kuchukulia kwa uzito swala la ibada na pia moja ya jambo mtendakazi anatakiwa kufahamu ambaye anaandaa ibada na mambo yote ni mtendakazi.

*Wakolosai 4:12-13SUV "Epafra, aliye mtu wa kwenu, mtumwa wa Yesu Kristo, awasalimu, akifanya bidii siku zote kwa ajili yenu katika maombi yake, ili kwamba msimame wakamilifu na kuthibitika sana katika mapenzi yote ya Mungu. Maana namshuhudia kwamba ana juhudi nyingi kwa ajili yenu, na kwa ajili ya hao walioko Laodikia, na kwa ajili ya hao walioko Hierapoli."*

Mtendakazi ana wajibu wa kukesha na kuomba zaidi ya kawaida, kufunga zaidi ya washirika wengine hivyo mtendakazi tambua kuwa ukawaida haupaswi kutajwa kwako kabisa.

***Dhabihu ya kupatikana (availability)***

Mtendakazi unapaswa kutambua kuwa hakuna mbadala wa raslimali watu. Mtendakazi ni kifaa ambacho hakiwezi kuwa “replaced” kwa namna yoyote ile. Moja ya jambo ambalo mtendakazi anapaswa kulitambua ni kwamba yeye ni raslimali inayopaswa kupatikana wakati wowote bila ya sababu yoyote ile; mtendakazi anapaswa kutokua na sababu ya

kukosekana kwenye jukumu ambalo anatakiwa kulitimiliza.

Mungu anatafuta watu wanaopatikana kwanza kabla ya kutazama uwezo wa watu hao (the availables over the ables)!

*Ezekiel 22:30SUV "Nami nikatafuta mtu miongoni mwao*, *atakayelitengeneza boma*, *na kusimama mbele zangu mahali palipobomoka*, *kwa ajili ya nchi*, *nisije nikaiharibu, lakini sikuona mtu."*

Tambua kuwa kupatikana kwako ni kigezo ambacho Mungu anakitumia kuongeza uwezo. Ukweli ni kwamba mtu asiyekuwepo kabisa na mtu asiyepatikana wanafanana maana wote hawatumainiki.

*Kutoka 2:11SUV "Hata siku zile, Musa alipokuwa mtu mzima, akatoka kuwaendea ndugu zake, akatazama mizigo yao. Akamwona Mmisri anampiga Mwebrania, mmojawapo wa ndugu zake."*

*Kutoka 3:11SUV "Musa akamwambia Mungu, Mimi ni nani, hata niende kwa Farao, nikawatoe wana wa Israeli watoke Misri?"*

Nimekua nikiwafundisha watumishi wa Mungu hasa wachungaji kwamba chagua kupatikana kuliko uwezo maana uwezo ni matokeo ya kupatikana.

***Dhabihu ya muda***

Kweli ni hii sehemu ambayo unawekeza muda mrefu ni unabii wa wapi unaelekea.

*Matendo 20:31SUV "Kwa hiyo kesheni, mkikumbuka ya kwamba miaka mitatu, usiku na mchana, sikuacha kumwonya kila mtu kwa machozi."*

*Luka 2:37SUV "Naye ni mjane wa miaka themanini na minne; haondoki katika hekalu, ila huabudu usiku na mchana kwa kufunga na kuomba."*

Muda ni kipimo cha kila jambo; muda unaamua mambo yanakuwaje hivyo

mtendakazi anapaswa kutambua kuwa kiwango cha muda anachokimimimina kwenye utumishi huamua matunda na matokeo kwenye eneo hilo. Nataka nilete kwako mtendakazi ya kwamba kiwango cha kuwekeza muda kweye utumishi kitambulike kama dhabihu. Yaani Zaidi ya kawaida; kweli ni hii, muda ni raslimali ambayo huwa haituzwi kwenye friji hivyo muda unaopita kwenye mikono yako uwekeze kwenye utumishi na kila kuwekeza kuna thawabu.

Hakika ni kwamba utavuna sawasawa na ulivyowekeza. Mungu huwa anatambua kiwango cha muda kama ni dhabihu yaani imehama kuwa ratiba na kuwa tabia na hapa

ndipo anatoa thawabu juu yako mtendakazi; kama ni kuomba omba mpaka iwe tabia, kama ni kusafisha kanisa safisha mpaka iwe tabia hapo utaona matokeo ya utumishi huo.

***Dhabihu ya utii***

Kwa namna ambavyo dunia ilivyo na inaenenda inawapa watu uhuru wa kulijadili na kutoa maoni kuelekea Neno la Mungu na hii inapelekea maafa makubwa kwa watu wengi hasa kutopokea matokeo ya aina yoyote ile na hivyo kuishia kuwa wanadamu wa kawaida.

Neno ndilo chanzo cha matokeo ya aina yoyote ile kwa mwanadamu, habari mbaya ni kwamnba hali hii imeingia kwenye

mioyo ya waamini kwa namna ya kimtego nayo ni kuanza kuwatii baadhi ya viongozi na kuwapuuzia wengine bila ya kujua wanajizuilia kupokea thawabu kwa kushindwa kuwapokea watumishi wa Mungu.

Hii ndiyo maana ya utii, mtendakazi anawajibu kuwapokea viongozi walio juu yake na walio chini yake kwa uzito bila ya kuwapuuzia wa upande mmoja maana hiyo ndiyo huzuilia ustawi wake.

*Wafilipi 2:8SUV "tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba."*

Kama mtendakazi mwitikio kwa Mungu ni utii, vivyo hivyo kwa watumishi mwitikio wangu ni kuwatii na si pungufu ya hapo; ni vizuri kukosea huku una nia njema kuliko kutokukosea huku una nia mbaya, yaani unajitahidi kufanya vizuri kwa lengo baya.

Uniruhusu tutazame aina za utii mbovu si kwa maana ya kupuuza utii mwema, tutazame utii;

i. Utii uliocheleweshwa

Aina hii ya utii inahusisha kutekeleza jambo ulililoagizwa na kiongozi lakini kwa kuwa nje ya kipimo cha muda, hivyo aina hii ya utii inapelekea mambo kutokea lakini kwa kiwango ambacho sio sahihi na

kilichokusudiwa. Mtendakazi mwenye nidhamu hii mara nyingi ataingia kwenye mgogoro na kiongozi wake kwa sababu anaamua muda gani atekeleze jambo aliloagizwa kitu ambacho sio sahihi kwenye utendaji wa kazi ya Mungu. Mara zote mtendakazi anawajibika kwa kiongozi wake kama inavyotakiwa sawasawa na matakwa ya kiongozi wake bila ya pungufu hata kidogo.

ii. Utii uliosogezwa mbele (usio wa wakati)

Aina hii ni utii ambao umefanywa lakini kwa kujipangia muda na wapi jambo lifanyike nje ya maelekezo ya kiongozi.

Mtendakazi mwenye aina hii ya utii huwa msukumo nyuma ya kutekeleza majukumu ni kwamba na yeye ana nguvu ya kutokeza matokeo sawa na kiongozi wake hivyo ndani yake hupanga namna gani afanye, kwa muda gani n ahata sehemu gania vyote hivyo anavitenda kinyume na kiongozi wake alivyotoa maelekezo.

iii. Utii pungufu

Mara nyingi aina hii ya utii imewapata watendakazi wengi na hata waamini wengi, inahusiana na kuchagua wa kuwatii na kuwaheshimu. Mtendakazi ambaye anachagua viongozi wa kuwatii anatuma ujumbe kuwa moyo wake hauko mahali

hapo, mara nyingi utaona mtendakazi ambaye anatii kwa kuchagua viongozi na kuwapuuzia wengine moyo wake wa utumishi huwa una changamoto na hii hupelekea kutekeleza baadhi ya majukumu na kupuuzia mengine wanayoagizwa na viongozi wengine.

iv. Utii uliolazimishwa

Utii huu unaambatana na namna ambavyo kiongozi anasukuma na kuwaingiza watu kwenye mtego wa kuogopa kwa maana ya mahusiano yao na kiongozi wao kua chini ya kipimo cha uoga. Mtendakazi anayehusiana na kiongozi wake katika

ngazi hii ya uoga na matokeo ya utii huu huwa ni kutozalisha matokeo sahihi ambayo kiongozi ameyakusudia.

## Dhabihu ya utalaam, ujuzi, maarifa na uzoefu

Kazi ya Mungu ni kazi ya kuheshimika hivyo namna ya kutenda mambo yanayohusiana na kazi hii inadai matumizi mazuri ya akili. Baada ya kupatikana Mungu anataka watu wataalam na wenye ujuzi hivyo watu wenye ujuzi na maarifa makubwa wanapaswa kupatikana kanisani na pia watumie viwekezo hivyo kumtumikia Mungu.

Mtendakazi mwenye ujuzi au ufahamu juu ya eneo lolote lile hakikisha ujuzi wako unatumika kwenye ujenzi wa nyumba ya Mungu nimekua nikiwaambia watendakazi kila ninapowafundisha kuwa “*unaruhusiwa kuja bila ujuzi, haupaswi kuendelea bila ujuzi*”

*Tito 3:13SUV "Zena, yule mwana-sheria, na Apolo, uwasafirishe kwa bidii, wasipungukiwe na cho chote."*

Kwenye kazi hii utagundua kuwa Mungu ana kawaida ya kutumia watu wenye nguvu kiufahamu, ujuzi, maarifa na hii ni kwa sababu kazi ya Mungu ni kazi ya thamani sana.

Mitume walitumika na watu wenye uwezo kwenye kila eneo na utaona ya kwamba Yesu alitumika na watu wenye nguvu na wenye ujuzi wa hali ya juu sana na hii ni kwa sababu thamani ya kazi hii sio ya kawaida.

Moja ya eneo ambalo mtendakazi anapaswa kuwa na uwezo mkubwa sana ni eneo la kuwaza; kiwango cha kuwaza huamua ni matokeo gani yanazalishwa na mtendakazi, nikupe siri hii kwenye serikali yoyote ile hakuna kodi ya kuwaza watu wanaruhusiwa kuwaza kwa kadri wanavyotaka na utagundua kuwa watu wanatofautishwa na kiwango wanavyowaza.

*“hakuna mpaka (boundary) kwenye kuwaza, waza unavyotaka kwa mapana yoyote yale”*

## Dhabihu ya mali

Dunia hii ina kawaida ya kuheshimu na kuitikia thamani gani inawekezwa kwenye kitu chochote kile. Niruhusu tutumie mfano wa kiwanda cha kuzalisha vinywaji kama soda; eneo kama hili utakutana na watu wengi na kila mmoja yuko *busy* hakuna ambaye amekaa tu bila jukumu na utagundua kila mmoja anavyokimbizana ni anazalisha chupa moja ya soda na hatimaye tunapata chupa nyingi za soda, utakutana na watu wa fedha, watu wanaobeba mizigo,

watu wanaoendesha mitambo, wakaguzi na wengine wengi hivyo ukiona umeshika chupa moja ya soda tambua nyuma ya chupa hiyo yenye soda kuna mikono ya watu wengi imehusika.

Sasa, nilikua nakujengea msingi sasa, unadhani watu wote hao wanafanya kazi kwa kujitolea? Unadhani nyuma yao hakuna familia? Kweli ni kwamba baada ya kipindi flani wanapokea posho hivyo kuwaza kufungua kiwanda ni vizuri lakini unapaswa kuwaza unaweza kuwalipa wafanyakazi hawa? Sasa, nikurejeshe kwenye taasisi ambayo ni kanisa, ukitazama vizuri utatambua kuwa kiwanda cha soda kinazalisha bidhaa ambazo ndani

yake hazina umilele, haziwezi kuokoa watu lakini utaona ni mali kiasi gani imewekezwa hapo hii ikupe kutafakari sana nini kiko nyuma ya maeneo haya mawili na eneo la pili ni kanisa hili limebeba mambo ya umilele na kuna maisha ya watu yanatengenezwa lakini ni kwa kiasi gani mali zimewekezwa hapo? Watu wameingia kwenye mtego na kuona kanisa ni eno ambalo linaweza kujiendea tu na linaweza kwenda hata kwa kutia huruma! Mungu aepushie mbali ufahamu huu kwako unayesoma haya.

Tambua kwamba eneo ambalo linapaswa kutumia mali kwa wingi na wala isionekane ni ajabu ni kanisani hivyo tambua kwamba

kazi ya Mungu ni kazi ya thamani sana na ni kazi ya kuthaminika sana na kuheshimika ni zaidi ya taasisi nyinginenzo ni zaidi ya kiwanda hivyo inadai mali zaidi ya jambo lolote lile.

*Kutoka 10:9-25 niruhusu tutazame mstari wa 25 tu SUV [25]"Musa akasema, Ni lazima utupe mikononi mwetu na wanyama wa dhabihu na wa sadaka za kuteketezwa, ili tupate kumchinjia Bwana Mungu wetu dhabihu."*

Kwa kutambua thamani ya kazi ya Mungu na mambo ya kwamba Mungu hapaswi kupangiwa vitu vya kupokea kama sadaka utamwona mtumishi wake Musa anadai

vitu vyote watoke navyo kwenda nchi ya ahadi hii ni kwa sababu vitu vyote ni mali ya Mungu hivyo anaweza kuhitaji chochote kama ibada kwake na sisi hatauwezi kumzuilia.

Hali ya maisha inaathiriwa na kwa namna gani utoaji kuelekea kazi ya Mungu ulivyo na hii ni kwa sababu mahali ambapo unaelekeza mali pana athiri hali ya moyo na hatimaye mambo yote ya maisha kwa ujumla wake.

*Mathayo 27:55SUV "Palikuwa na wanawake wengi pale wakitazama kwa mbali, hao ndio waliomfuata Yesu toka Galilaya, na kumtumikia."*

*Luka 8:3SUV "na Yoana mkewe Kuza, wakili wake Herode, na Susana, na wengine wengi, waliokuwa wakimhudumia kwa mali zao."*

Hakuna mtendakazi ambaye hana kitu cha kutoa kwenye nyumba ya Mungu, na kwa mtendakazi kiwango cha utoaji kinapaswa kutambulika kama dhabihu.

## Dhabihu ya nguvu

Matumizi ya nguvu ni jambo ambalo Mungu analitarajia kwenye maisha ya mtendakazi, matumizi ya nguvu za mwili ni kufanya kitu na kumaanisha kile unachokifanya. Pia maana nyingine ya

nguvu ni kulazimisha matokeo (aggression) yaani kusukiumuma vitu mpaka vitokee.

*Yeremia 48:10SUV "Na alaaniwe mtu afanyaye kazi ya Bwana kwa ulegevu; na alaaniwe auzuiaye upanga wake usimwage damu."*

*Mhubiri 10:18SUV "Kwa sababu ya uvivu paa hunepa; Na kwa utepetevu wa mikono nyumba huvuja."*

Kuna mambo hayatokei ni kwa sababu ya uvivu wa mtu mmoja; uhakika ni huu kila jambo unaloliona ni matokeo ya mikono ya mtendakazi ambaye amehusisha nguvu katika utendaji kazi. Tambua hili ya kwamba kazi ya Mungu ni kazi kubwa

hivyo inadai mikono mingi na yenye nguvu kwenye kuyaendea mambo yanayoihusu kazi hii. Nimewahi kumsikia mtumishi wa Mungu Bishop David Oyedepo anasema *kazi hii mnayoiona imesimama imegharimu damu ya Yesu na pia damu yangu.*

## Dhabihu ya uhai (maisha)

Mara zote dunia ina hasira kubwa sana kinyume cha kazi ya Mungu na huwa ninasema kwamba ni sahihi watu wa aina nyingine kumiliki mambo mazuri lakini utaona chuki kueleka mambo mazuri ndani ya kanisa.

Kwa wakati wote Imani iliyowekwa ndani yetu kama waamini sio jambo la kiutani tambua kuna vita kubwa sana kupinga Imani hii, hivyo maisha ya wokovu mara zote ni vita na sio vita ndogo ni kubwa sana maana utaona hasira na chuki ya dunia kuelekea kanisa kwa namna mbalimbali.

Dunia iko kazini kuhakikisha inaangusha watumishi wa Mungu na utaona vita mbalimbali hasa ya uzushi ni kali sana kuwaelekea watumishi wa Mungu na lengo la vita hiyo ni kuwaangusha kwa kutumia mbinu ambayo inawaanika watumishi wa Mungu kwa kuwatafutia mambo yasiyo ya kweli na kuyafanya kwamba ni kweli (ukweli nusu) na mara nyingi mtendakazi

inawezekana umeingia kwenye mtego wa kuwazungumzia watumishi wa Mungu kwa namna isiyofaa bila ya kujua unatenda kazi na shetani moja kwa moja.

*2 Wakorintho 11:14SUV "Wala si ajabu. Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru."*

Nimekua nikishauri watendakazi kanisa ninalolichunga kama utaona kwako pia ni jambo jema ni vyema ukafanya hivyo *"jambo lolote ambalo hauna uhakika nalo kumwelekea mtumishi wa Mungu ni vyema ukafunga kinywa na usiliongelee na pia jambo ambalo una uhakika nalo na ni ovu*

*mwitikio wako ni maombi kumwelekea mtumishi huyo*”.

Inamgharimu Mungu muda mrefu na rasilimali nyingine mbalimbali kuandaa mtumishi, hivyo kama mtendakazi wajibu wako ni kumlinda kiongozi wako hakikisha uhai wake namaanisha pumzi ya uhai iko salama, hakikisha kiongozi wako anaweza kuendelea na majukumu bila ya kuwa na wasiwasi na uhai wake, hakikisha familia yake iko salama mbali na aina yoyote ile ya mambo yanayoweza kuwadhuru.

*Warumi 16:3-4SUV “Nisalimieni Priska na Akila, watenda kazi pamoja nami katika Kristo Yesu; waliokuwa tayari hata*

*kukatwa kichwa kwa ajili ya maisha yangu; ambao ninawashukuru, wala si mimi tu, ila na makanisa ya Mataifa yote pia; nisalimieni na kanisa lililomo katika nyumba yao*."

Hapa Priscilla na Akila walikua tayari kumlinda mtumishi wa Mungu kiasi cha kuutoa uhai wao, mtendakazi anapaswa kujua kwamba usalama wa kiongozi wake ndio usalama wake hivyo usipuuzie usalama wa kiongozi wako na ifike hatua mtendakazi uwe tayari kufa pamoja na kiongozi wako.

*Mathayo 26:35SUV "Petro akamwambia, Ijaponipasa kufa nawe, sitakukana kamwe. Na wanafunzi wote wakasema vivyo hivyo."*

*Ufunuo 2:10SUV "Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima."*

Ukweli ni kwamba mtendakazi ambaye yuko kutoa uhai wake kwa ajili ya injili mtendakazi huyu yuko tayari kutoa jambo lolote lile.

## Dhabihu ya mambo yanayokupendeza na kukupa raha

Dhabihu inahusisha kugandamiza matakwa yanayoufurahisha moyo.

*Luka 9:59-62SUV "Akamwambia mwingine, Nifuate. Akasema, Bwana, nipe ruhusa kwanza niende nikamzike baba yangu. Akamwambia Waache wafu wawazike wafu wao; bali wewe enenda ukautangaze ufalme wa Mungu. Mtu mwingine pia akamwambia, Bwana, nitakufuata; lakini, nipe ruhusa kwanza nikawaage watu wa nyumbani mwangu. Yesu akamwambia, Mtu aliyetia mkono*

*wake kulima, kisha akaangalia nyuma, hafai kwa ufalme wa Mungu."*

Katika eneo hili nataka nitambulishe desturi ya wayahudi kuhusu taratibu zao za maziko na hapa tutapata nini Yesu alikua anakimaanisha kwa ndugu huyu.

Wayahudi walitumia muda wa miezi 12 kukamilisha zoezi la maziko na kila wakati kwa vipindi vyake walifanya jambo kuuhusu mwili au kaburi hilo, hivyo ilimbidi ndugu huyu apatikane kwa muda wa miezi 12 na baada ya hapo aweze kuungana na Yesu katika utumishi. Kutokea hapo tunapata mambo haya, jukumu la maziko sio linapuuzwa bali kwa

kulinganisha matokeo yanayozalishwa na jukumu hilo linaonekana halina maana kwa kulilinganisha na kazi ya utumishi ambayo ngudu huyu ameitiwa kwa hiyo, hivyo Yesu anatuma ujumbe ya kwamba muda wa miezi 12 katika utumishi sio sawa na miezi 12 katika shughuli ya maziko na utaona ya kwamba jukumu hili la maziko kwa jamii ya wayahudi limebadilika sasa na kuwa jambo linalowapa kukaa bila kufanya shughuli nyingine hiki ndicho Yesu anapambana nacho kwa Marko.

Mtendakazi ambaye anawekeza muda kwenye mambo yanayomfurahisha nje ya utumishi na hapa simaanishi mambo yanayokufanya ufurahi tu bali

yanayochukua muda wako kwa uendelevu na sasa yamekua ni sehemu yaani tabia ya maisha yako hataweza kuzalisha matokeo thabiti kwenye ufalme wa Mungu.

Mtendakazi unapaswa kuweka mbele kazi ya Mungu zaidi ya mambo yote wekeza muda na kila kitu kwa ajili ya kazi ya Mungu na si vinginevyo.

## Dhabihu ya ufuasi

Mwanadamu ni kiumbe ambaye kwa asili anapenda kuwa huru, hapendi kuwajibishwa, hapendi maongozo kabisa hivyo mwanadamu mara zote akipewa

nafasi ya kuwa huru utagundua ni nyakati ambazo alimsahau Bwana.

Hivyo mwanadamu kimsingi anapaswa kuwa chini ya maongozi, jambo la ufuasi sio jambo la kwa mwanadamu na utaona linahusisha kujikabidhi kwa mtu mwingine na kuruhusu maisha yako yaongozwe na kusimamiwa na mtu mwingine.

Ufuasi ni swala ambalo sio la kulazimishwa linadai utayari ambao umechotwa kwenye moyo hivyo mtendakazi anapaswa kuwa tayari kulipia gharama hii ya utayari kwa kuwa chini ni kufuaswa na kiongozi wake

*1 Wakorintho 4:14-16SUV “Siyaandiki hayo ili kuwatahayarisha; bali kuwaonya*

*kama watoto niwapendao. Kwa kuwa ijapokuwa mna waalimu kumi elfu katika Kristo, walakini hamna baba wengi. Maana mimi ndimi niliyewazaa katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili. Basi, nawasihi mnifuate mimi."*

**Kuhusu Mwandishi:**

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**
Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: Pastor James Kalekwa

Instagram: @pastorjameskalekwa

Youtube: Pastor James Kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

NEW VINE CHURCH | Dodoma



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

## Ratiba za Ibada

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni
**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor ,Priscilla na Butogwa. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa

+255 754 917 764

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

MchungajiJK

+255 754 917 764

jameskalekwa.com